



KANISA LA KIINJILI YA KILUTHERI TANZANIA
DAYOSISI YA KASKAZINI KATI
SHULE YA SEKONDARI ENABOISHU
S.L..P. 3120, ARUSHA.
SIMU: 0755 287953 /0784-322068 , 0755- 854325

FOMU YA BWENI PC NA A – LEVEL 2019

Fomu hii ni kwa ajili ya wanafunzi wanaomba nafasi ya kuwa bweni tu

(A) Ndugu Kidato cha mwaka 2018/2019

Napenda kukufahamisha kwamba ombi lako la kupatiwa nafasi ya kulala Bweni katika shule hii limekubaliwa. Unatakiwa kufika Bwenini tarehe

TARATIBU ZOTE ZA SHULE - Angalia fomu ya kuijunga.

(B) MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA NA WANAFUNZI WA BWENI

1. Mwanafunzi hatapokelewa Bwenini hadi atakapolipa karo yote ya muhula.
2. Mwanafunzi wa Bweni la **wavulana** hatakiwi kuleta godoro
3. Kila Mwanafunzi wa Bweni anatakiwa alete mto, taulo, blanketi, ndoo, brash ya viatu , vifaa vya usafi binafsi na vyombo vya kulia chakula yaani sahani, kikombe, kijiko na Bakuli.
4. Mwanafunzi akibainika kuwa na mwenendo mbaya au kutofuata taratibu za Bweni atafukuzwa bwenini mara moja. Mf. Utoro, kulala nje ya Bweni
5. Kila mwanafunzi anatakiwa awe na fedha za kutosha (pocket money) kwa ajili ya matumizi binafsi. Fedha hizi zitunzwe kwa Katibu muhtasi (secretary) wa mkuu wa shule.
6. **Mwanafunzi ambaye sio wa Bweni haruhusiwi kamwe kuingizwa bwenini**
7. Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani zaidi ya zile alizoagizwa.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na **SIMU AU RADIO** bwenini.
9. Siku ya kutembelewa wanafunzi wa Bweni na Mzazi/Mlezi ni siku ya kikao cha wazazi wote , siku ya mahafali ya kidato cha sita , au kidato cha nne au mahafali ya dini tarehe mtajulishwa.
10. Ni marufuku kwa mwanafunzi ye yeyote kutembelewa na mgeni wakati wa masomo.
11. Kila mwanafunzi wa bweni anatakiwa kuwa na tochi.
12. Taratibu na sheria zingine za Bweni zinapatikana kwenye maelezo ya kuijunga na shule na kwenye ubao wa matangazo.
13. Mwanafunzi wa Bweni la **Wasichana hatakiwi kuleta godoro**
14. Kuhudhuria ibada siku za jumapili au siku nyingine kulingana na utaratibu wa imani yako.
15. Kila mwanafunzi awe na vitabu vya Ibada mfano Biblia takatifu, Tumw abudu Mungu wetu, Misale ya waumini,Tenzi za rohoni n.k.
16. Ni marufuku kutembelea nyumba za walimu bila ruhusa ya Mkuu wa shule.
17. Matumizi sahihi ya bweni kwa kuzingatia viwango vya ufaulu (pass marks)
18. Nidhamu , Upendo, na ushirikiano sahihi ni kitu muhimu vinginevyo utapoteza nafasi ya kuwa bwenini.
19. Tatizo lolote litokeapo liripotiwe kwa Patron/Matron au Walimu walezi wa Bweni
20. Mwanafunzi wa bweni anatakiwa kuleta Jembe lenye mpini.

(c) *KARIBU ENABOISHU KWA MALEZI BORA.*

**GODWIN JOHN
MKUU WA SHULE**

Tarehe